

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO

Simu: +028 2228007  
Fax Na.: +028 2228007  
Baruapepe:  
ded@chatodc.go.tz  
Website: [www.chatodc.go.tz](http://www.chatodc.go.tz)



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (V)  
S.L.P. 116,  
CHATO – GEITA.

Kumb.Na.CDC/05/20/VOL.II/03

Tarehe: 25/11/2019

## YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya wilaya ya Chato kuitia Shirika la MDH (Management and Development for Health) inawatangazia nafasi za Ajira za Mkataba kwa mtumishi **1** ambaye atafanya kazi za (**Data Officer**). Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Chato anakaribisha maombi kwa Watanzania wenyе sifa za kujaza nafasi kama ilivyoorodheshwa katika tangazo hili:

### DATA OFFICER - NAFASI MOJA (1)

#### SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne , cha Sita au Shahada
- ii. Awe raia wa Tanzania
- iii. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na si zaidi ya mika 45.
- iv. Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo stahiki ya nafasi anayoomba.
- v. Awe na uwezo wa kutunza siri za wateja anaowahudumia
- vi. Awe tayari kufanya kazi na kuishi katika mazingira yoyote hasa vijijini
- vii. Awe na ujuzi katika fani ya takwimu (statistics)
- viii. Awe na ujuzi katika fani ya utunzaji kumbukumbu za kielektronik za afya (Health Records Management)
- ix. Awe na ujuzi katika fani ya teknolojia ya habari za mawasiliano (ICT)
- x. Wenyе usoefu katika matumizi sahihi ya takwimu na mifumo ya kutolea taarifa watapewa kipaumbele.

#### MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kukusanya takwimu za upimaji wa VVU na kuingiza kwenye mfumo (CTC2 DATABASE)
- ii. Kutunza takwimu na taarifa zote zilizomo kwenye mfumo
- iii. Kufanya uhakiki wa takwimu katika viashiria vya ukimwi kila mwezi
- iv. Kupanga mafaili kwa kufuata mtiririko
- v. Kuandaa chati / grafu zinazoonesha utendaji wa kituo katika viashiria vya VVU/ UKIMWI kwa kila mwezi na robo mwaka na kuziweka kwenye ubao wa matangazo
- vi. Kurekebisha taarifa zilizoingizwa kimakosa kwenye mfumo (Running Validation Check).
- vii. Kutoa taarifa / mapendekezo juu ya mtiririko wa takwimu na uingizwaji wa takwimu kwenye mfumo wa CTC2 DATA BASE kwa viongozi wanaokusimamia.

- viii. Kutekeleza majukumu mengine utakayopangiwa na viongozi wako wa kazi.

### **MSAHARA**

Mwajiriwa atapata mshahara wa kiwango cha Tsh. 680,000/= kwa mwezi

### **MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18 usiozidi miaka 45
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, kitaalamu pamoja na nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- v. Testimonials”, “**Provisional Results**”, “**Statement of results**”, hati za matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA**
- vi. Awe hajawahi kupatikana na hatia kuwa na makosa yoyote ya jinai hasa wizi au rushwa
- vii. Viambatanisho vyote vibanwe vizuri kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.
- viii. Mwombaji aambatanishe picha moja pasporti size ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma.

**NB:** Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza na ya tumwe kuitia posta au kuwasilishwa moja kwa moja ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji chato kwa anuani ifuatayo: -

### **MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**SLP.116**

**CHATO -GEITA**

Mwisho wakupokea barua za maombi ni **Tarehe 05 Disemba, 2019 saa tisa na nusu alasiri (9:30)**.

Imetolewa na;



E.L.Mwaiteleke

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**CHATO.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

S. L. P. 116

CHATO